TANGAZO LA SERIKALI NA. 74 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KITALI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Kitali ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 590898MS, 8979268KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ $89^0$ 51' 33.45 MS kwa umbali wa kilomita 1.86 hadi kwenye alama ya mpaka namba B yenye majira-nukta 592761MS, 8979272KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa KS $3^0$ 27' 18.27 MS kwa umbali wa kilomita 3.93 hadi

*Tangazo La Serikali Na. 74 (Linaendelea)*

kwenye alama ya mpaka namba C yenye majira-nukta 592998MS, 8975345 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS $65^0$ 17' 38.31MG kwa umbali wa kilomita 0.59 hadi kwenye alama ya mpaka ya namba D yenye majira-nukta 592453MS, 8975095 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ $47^0$ 02' 59.74 MG kwa umbali wa kilomita 1.09 hadi kwenye alama ya mpaka namba E yenye majira-nukta 591648MS, 8975844 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea katika uelekeo Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ $32^0$ 48' 43.89 MG kwa umbali wa kilometa 0.89 hadi kwenye alama ya mpaka namba F yenye majira-nukta 591166 MS, 8976592 KZ;baada ya hapo unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ $72^0$ 20' 59.46 MS kwa umbali wa kilomita 0.38 hadi kwenye alama ya mpaka namba G yenye majira-nukta 590803MS, 8976707KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ $2^0$ 08' 41.12MS. kwa umbali wa kilomita 2.56 hadi kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 590898MS, 8979268KZ unapoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*